



ACP-EU Culture Programme: Ignite Culture

Maelezo Ya Jumla

Ignite Culture ni kituo kipya na cha kuisimua cha ruzuku kwenye sekta za kitamaduni na ubunifu katika nchi 14 za Afrika Mashariki! Mfuko huu wa ruzuku unaolenga Afrika Mashariki ni sehemu ya Mpango wa Utamaduni wa ACP-EU wa kimataifa ambao unatekelezwa na, kwa ushirikiano na [Baraza la Uingereza la Kenya](#) na mchango wa kifedha kutoka kwa Umoja wa Ulaya, na kwa msaada zaidi kutoka kwa [Muungano wa ACP](#) (yaani mataifa ya Afrika, Karibea na Pasifiki).

Maelezo ya jumla

Ignite Culture ni kituo kipya na cha kuisimua cha ruzuku kwenye sekta za kitamaduni na ubunifu katika nchi 14 za Afrika Mashariki! Mfuko huu wa ruzuku unaolenga Afrika Mashariki ni sehemu ya Mpango wa Utamaduni wa ACP-EU wa kimataifa ambao unatekelezwa na [HEVA](#), kwa ushirikiano na [Baraza la Uingereza la Kenya](#) na mchango wa kifedha kutoka kwa Jumuiya ya Ulaya, na kwa msaada zaidi kutoka kwa [Muungano wa ACP](#) (yaani mataifa ya Afrika, Karibea na Pasifiki).

The ACP-EU CULTURE Programme is an initiative funded by the European Union (EU) and implemented by the Secretariat of the Organisation of African, Caribbean and Pacific States (OACPS).



Ufadhili huu utawasaidia waliofanikiwa kupewa fedha kuanzisha shughuli na miradi itakayowafaidi wao wenyewe, na kuendeleza shughuli za kitamaduni na usaidizi katika jamii zao lengwa. Pia itasaidia kuhakikisha kuwa juhudi zao zinakuwa endelevu zaidi.

Pamoja na kuwasaidia wahusika katika ubunifu na utamaduni wao ili kukuza biashara zao, kuingia na kupanua masoko yao kidijitali, na kuboresha sehemu zao za kazi na ushirikiano, mfuko huu wa ruzuku utaimarisha juhudi za kujenga maarifa, na kuunda njia za kuwezesha mazingira bora ya kufanya kazi kwa biashara za ubunifu.

Kupitia ufadhili wa ruzuku ya hadi Yuro 180,000 kwa kila mwombaji, msaada huu wa kifedha wapaswa kuelekezwa kwa shughuli zifuatazo:

- kuongezeka na kuboreshwa kwa uzalishaji wa bidhaa na huduma za kiubunifu na kitamaduni, kujenga maarifa,
- kuboresha miundombinu, vifaa na programu,
- kuboresha upatikanaji wa fedha na sera tegemezi na mazingira bora ya biashara,
- kupanua ufikiaji wa masoko ya ndani, ya kikanda na ya kimataifa, na vile vile
- kuboresha mwonekano kwa watendaji wabunifu na kitamaduni na kazi zao katika eneo lote la Afrika Mashariki.

Katika kipindi cha miezi 40 ijayo, Ignite Culture itakuwa wazi kwa wenye kutuma maombi nchini Burundi, Visiwa vya Komoro, Djibouti, Eritrea, Ethiopia, Kenya, Madagaska, Mauritius, Rwanda, Ushelisheli, Somalia, Sudan, Tanzania na Uganda.

Wito wa kuwasilisha maombi uko wazi kuanzia Jumatatu 9 Agosti 2021!

Wanaostahiki

Wenye vipaji vya ubunifu waliosajiliwa na wafanyabiashara (biashara zilizohudumu kwa angalau miezi 12) nchini Burundi, Visiwa vya Komoro, Djibouti, Eritrea, Ethiopia, Kenya, Madagaska, Mauritius, Rwanda, Ushelisheli, Somalia, Sudan, Tanzania na Uganda watakaribishwa kuomba ruzuku ya hadi Yuro 180,000 kwa kila mwasilishaji maombi.

Sekta za CCI zitakazozingatiwa ni pamoja na: Turathi za Kitamaduni na Asili, Utendaji na Sherehe, Miundombinu ya Kitamaduni, Sanaa ya Uonekanaji na Ufundi, Vitabu na Wanahabari, Vyombo vya Habari vya kutazamwa na kusikika, Huduma za Usanifu na Ubunifu, Elimu ya Ubunifu na Utamaduni na Turathi za Kitamaduni Zisizogusika.

The ACP-EU CULTURE Programme is an initiative funded by the European Union (EU) and implemented by the Secretariat of the Organisation of African, Caribbean and Pacific States (OACPS).



Utaratibu wa kuwasilisha maombi

Ignite Culture itaanza kupokea maombi **Jumatatu, Agosti 9, 2021**. Wawasilishaji maombi wote ambao wamejaza fomu ya maombi watapokea arifa kwamba maombi yao yamepokelewa.

Wale ambao maombi yao yalifanikiwa watapitia hatua kadhaa za tathmini, ikiwemo mchakato wa kuhakikisha uhalali wa shughuli zao. Kisha watapitia hatua ya ukaguzi wa kifedha ambayo itatathmini uwezo wa biashara husika au taasisi, na mradi uliopendekezwa, ili kuchukua kiwango cha pesa za ruzuku kilichoombwa. Hatua ya mwisho itakuwa kuweka mikataba, na kisha kutangaza waliohitimu.

Habari zaidi zaja hivi karibuni!

Ukurasa wa viungo vya mitandao ya kijamii

[Twitter](#), [Facebook](#), [Instagram](#)
